

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KABL
LA YA KUPANDA UYOGA**

1. Hakikisha nyumba ya Uyoga imejengwa katika mazingira mazuri / safi.
2. Hakikisha usafi unafanyika kuzunguka nyumba ya Uyoga.
3. Sehemu ya kuchemshia takataka (mbolea) iwe tofauti na sehemu ya kupandia Uyoga.
4. Hakikisha kabla hujagusa mbolea yako unasafisha mikono kwa kutunia pamba ili yoweke wa spiriti.
5. Mifuko ikishambuliwa na magonjwa, itoe kwenye nyumba na itupe mbali kuzuia maambukizi.
6. Nyumba ya Uyoga isitumike kwa kitu kiugine.

KUANDAA SUPU YA UYOGA

VIFAA

Uyoga mbichi au mkavu.
Tui la karanga.
Nyanya, karoti na pilipili hoho.
Maziwa yasiyoganda (fresh milk)

HUTUA

Katakata vipande vidogo vya uyoga.
Osha nyanya, karoti na pilipili hoho
Katakata kitunguu.
Katakata nyanya, karoti na pilipili hoho.
Kaanga kitunguu.
Ongeza nyanya, karoti na pilipili hoho na endelea kukaanga.
Ongeza tui la karanga na uendeleo kukoroga.
Ongeza maziwa kama yapo kiasi kulingana na wingi wa uyoga unao andaa.
Ongeza maji kulingana na kiasi cha karanga ulichotumia ili supu yako isiwe nzito sana wala rojorojo sana.
Ongeza uyoga kwenye mchanganyiko huo.
Waweza kuongeza pilipili na ndimu, kulingana na utashi wako.
Sasa supu yako itakuwa tayari.

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA

NASI:

SIMU: 028 2220921

Email: vanillaorganisation@yahoo.com

P.O. Box 1753

BUKOB.

KILIMO CHA UYOGA



Chama cha Maendeleo ya Wakulima

P.O. Box 1753 Bukoba

Tel office: 028-2220921

Tel shop: 028-2221128

E-mail: vanillaorganisation@yahoo.com

UTANGULIZI

Uyoga ni mmea kama mimea mingine ambao upo katika kundi la mimea aina ya fangasi.

Aina nyingi za fangasi zina seli kama za mimea mingine. Lakini fangasi hazina uwezo au tabia ya kutumia nguvu ya jua kwa kujitengeneza chakula chake kwa vile hazina rangi ya kijani. Hivyo Uyoga hutegemea chakula chake kilichotengenezwa na viumbe wengine kama alivyo binadamu na wanyama.

KUOTESHA UYOGA:

MAHITAJI:

- (a) Ni lazima uwe na kibanda ambacho kina sehemu mbili -chumba kidogo cha giza na chumba cha mwanga.
- (i) Chumba cha giza-Ni chumba cha kuweka mifuko ya takataka iliyochanganywa na spawn yaani mbegu za uyoga kwa muda wa wiki mbili hadi tatu.
- (ii) Chumba cha Mwanga -Hiki ni chumba ambacho mifuko uhamishiwa na ndipo uyoga huvunwa. Chumba hiki kiwe na mwanga ambao unakuwezesha kusoma gazeti.

NB: Kibanda kivezekwe kwa nyasi ili kupunguza joto.

(b) Unyevunyevu katika nyumba ya kuoteshea uyoga

- (i) Kwenye chumba cha giza si lazima kunyunyizia maji, ila joto liwe 25°C
- (ii) Chumba cha mwanga kinahitaji kunyunyizwa maji sakafuni ili uyoga uote ambacho ni 20°C -24°C.
- Unyevunyevu: chumba cha giza 60%
 - Chumba cha mwanga -75%
- (c) Takataka (substrates) hiki ni chakula cha uyoga

Zipo aina mbalimbali za takataka, lakini aina zifuatazo ni nzuri zaidi:

- (i) 'Ebikamulo' mabaki ya kutengeneza togwa ya ndizi
- (ii) Mabaki ya maharage baada ya kupula
- (iii) Mabaki ya mpunga
- (iv) Pumba za pamba
- (v) Majani ya matete haya ni makavu

NB: Takataka hizi hulowekwa usiku kucha, baada ya kukatwa katwa katika vipande vya inchi 2-3

- Tumia pipa lililowekwa lita 20 za maji na zifunikwe na vipande vya mashina ya migomba ikifuatia magunia kufunika kuta za pipa
 - Weka takataka kwenye pipa baada ya kuzichuja na kuziweka kwenye turubai safi.
 - Unaweza kuchanganya chokaa nusu sahani kila baada ya kupakia takataka debe mbili.
- (d) Mbegu za Uyoga (spawn)
- (e) Mifuko ya plastiki myeupe na myeusi yenye uwezo wa kubeba kilo 4-5
- (f) Vifaa vya kutolea mbegu kwenye chupa, kwa mfano: spoke, kijiko kidogo cha maabara au kijimti chembamba kilichokisafi.
- (g) Sahani ya kuwekea mbegu kabla ya kupanda
- (h) Pamba na spriti kwa ajili ya kusafishia mikono ya vyombo ili kuuwa wadudu wanaoweza kushambulia uyoga
- (i) Vipande vya shina la mgomba vyenye urefu wa futi moja na vilivyogawanywa kwa kufuata masharti ya upandaji wa uyoga na ikiwa umetumia takataka nzuri unaweza kuvuna kiasi cha asilimia 70% ya uzito wa mifuko.

FAIDA ZA KULA UYOGA:

1. Uyoga unayo protini asilimia 4(4%)
2. Uyoga unayo wanga asilimia 3.8 (3.8%)
3. Uyoga una wanga kidogo. Hivyo tunahauri utumiwe na wagonjwa wa kisukari
4. Uyoga una chembe chembe zinazozuia kukua kwa seli za kansa
5. Uyoga una vitamini A,B,C na D. Chembe chembe za vitamini D zina sifa za kusafisha mishipa ya damu.
6. Uyoga una mafuta kidogo kiasi cha asilimia 0.2 (0.2%)
7. Uyoga unayo sifa ya kuwa na chembe chembe za dawa kwa mfano:-
 - (a) Sifa ya kuwa na Antibiotiki.
 - (b) Sifa ya kupunguza kukua kwa seli za kansa.
 - (c) Sifa ya kupambana na baadhi ya Virusi
 - (d) Sifa ya kupambana na magonjwa ya ngozi
 - (e) Sifa ya kurekebisha msukumo wa damu.